Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Ananiudhi mimi mwanadamu, anatukana nyakati na mimi ndiye nyakati, ninaugeuza usiku na mchana

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Ananiudhi mimi mwanadamu, anatukana nyakati na mimi ndiye nyakati, ninaugeuza usiku na mchana".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Hadithil Kudsi: Ananiudhi na ananishusha hadhi mwanadamu anayetukana na kusema vibaya wakati wa kufikwa na matatizo na machukizo; kwa sababu yeye Mtukufu ndiye mpangiliaji peke yake na muendeshaji wa yote yanayotokea; kutukana nyakati ni kumtukana Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na kutukuka, na nyakati ni kiumbe na kinaendeshwa, yanatokea matukio ndani yake kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/66284